

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA**



## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa nafasi za kazi ili kuboresha utendaji kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa ufanisi zaidi.

### **1.0 Mtendaji wa Kata III – (Nafasi 3)**

#### **1.1 Ngazi ya Mshahara: TGS C**

#### **1.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Mtendaji wa Shughuli zote za Kata.
- (ii) Mtunzaji wa kumbukumbu zote za Kata za vikao vyta Kata.
- (iii) Kuhamasisha utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya Kata.
- (iv) Mlinzi wa amani katika Kata.
- (v) Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo katika Kata.
- (vi) Kupanga na kuhakikisha kuitishwa kwa ratiba za vikao vyta Kamati ya Maendeleo ya Kata.
- (vii) Kuandaa taarifa mbalimbali za Kata.
- (viii) Mfutiliaji wa miradi ya Kata na kutoa taarifa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

#### **1.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania
- (ii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye Stashahada katika fani ya Utawala, Sheria, Rasilimali watu, Maendeleo ya jamii au Usimamizi wa fedha kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- (iii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

## **2.0 Mtendaji wa Kijiji III – (Nafasi 1)**

### **2.1 Ngazi ya Mshahara: TGS B**

#### **2.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Mtendaji wa Shughuli zot za Kijiji.
- (ii) Mtunzaji wa kumbukumbu zote za kijiji za vikao vya Kijiji pamoja na hati ya kuandkishwa Kijiji,mali za kijiji,na rejestra ya kijiji.
- (iii) Kuhamasisha utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Mlinzi wa amani katika Kijiji.
- (v) Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo katika Kijiji.
- (vi) Kupanga na kuhakikisha kuitishwa kwa ratiba za vikao vya mukutano mkuu na Halmashauri ya Kijiji.
- (vii) Kuandaa taarifa mbalimbali za Halmashauri ya kijiji kwa ajili ya mukutano mkuu wa kijiji.
- (viii) Msimamizi wa mapato na kodi za kijiji.
- (ix) Mfuatiliaji wa miradi ya kijiji na kutoa taarifa kwenye halmashauri ya kijiji.

#### **2.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania
- (ii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye cheti cha fani ya Utawala,Sheria,Rasilimali watu,Maendeleo ya jamii au usimamizi wa fedha kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- (iii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

## **3.0 Msaидizi wa Kumbukumbu II (Nafasi 1)**

### **3.1 Ngazi ya Mshahara: TGS B**

#### **3.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.
- (ii) Kudhibiti upokeaji,uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- (iii) Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka.
- (iv) Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika masjala.
- (v) Kutunza,kudhibiti na kutoa kumbukumbu.
- (vi) Kutambua na kutafuta kumbukumbu/nyaraka katika masjala.

### **3.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania
- (ii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye cheti cha utunzaji kumbukumbu katika fani ya Masjala.
- (iii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

### **4.0 Dereva II – (Nafasi 1)**

#### **4.1 Ngazi ya Mshahara: TGS B**

##### **4.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Kuendesha magari.
- (ii) Kuhakikisha gari na vyombo vyake viko hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- (iii) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari .
- (iv) Kutunza na kuandika daftari la safari (Log book) kwa safari zote.

##### **4.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania.
- (ii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- (iii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye Leseni ya daraja C ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari.
- (iv) Uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali.
- (v) Mwenye cheti cha majoribio ya ufundi daraja la pili.

### **5.0 Msaidizi wa Jikoni II – (Nafasi 4)**

#### **5.1 Ngazi ya Mshahara: TGOS B**

##### **5.2 Majukumu ya kazi:**

- (i) Kusafisha vyombo vyakupikia
- (ii) Kusafisha vyombo vyakulia chakula
- (iii) Kusafisha sehemu ya kulia chakula
- (iv) Kuwatayarishia wapishi/waandazi vifaa vyakazi
- (v) Kusafisha maeneo ya kupikia

##### **5.3 Sifa za Mwombaji**

- (i) Awe Mtanzania

- (ii) Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- (iii) Awe mhitimu wa kidato cha nne au cha sita mwenye cheti cha Mafunzo ya Uhudumu wa jikoni kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali..

### **MAELEKEZO YA JUMLA**

1. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma yake.
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Andika nafasi uliyoomba juu ya bahasha yenye barua yako ya maombi.
4. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06/09/2017 saa 9:30 alasiri.
5. Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti: [www.mkingadc.go.tz](http://www.mkingadc.go.tz)
6. Maombi yatakayowasilishwa moja kwa moja na mwombaji kwa mkono hayatafanyiwa kazi.
7. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ya :

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**

**S.L.P 6005,**

**TANGA.**